



Bi. Ramona Tyson, Msimamizi

SWAHILI

Bw. Marshall D. Orson, Mwenyekiti wa Bodi

Bi. Vickie B. Turner, Mwenyekiti Msaidizi

Bw. Stan O. Jester

Dkt. Michael A. Erwin

Bi. Allyson Gevertz

Bw. Dijon DaCosta

Dkt. Joyce Morley

Mawasiliano ya Vyombo vyo Habari:

Portia Kirkland

Mkurugenzi wa Muda wa Mawasiliano

portia_kirkland@dekalbschoolsga.org

678-427-4898

Carla Parker

Mtaalamu wa Mawasiliano

carla_parker@dekalbschoolsga.org

404-734-1717

Kwa Toleo la Moja kwa Moja

Jumane, 30 Juni 2020

Cheryl Watson-Harris Anaanzisha Kipindi Kipya katika Shule za Wilaya ya DeKalb na Hafla ya Kuapishwa Kesho.

Hafla ya Watson-Harris ya kuapishwa itakuwa ikipeperushwa moja kwa moja kuanzia 9:30 asubuhi.

STONE MOUNTAIN, Ga. — Msimamizi mteule Cheryl Watson-Harris, atachukua rasmi jukumu la usimamizi wa Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb (DCSD) wakati ataapishwa kesho, Julai 1, na Jaji Mheshimiwa Gregory A. Adams wa Mahakama Makuu ya DeKalb katika Robert R. Freeman Administrative Complex.

Watson-Harris atajiunga na Mwenyekiti wa Bodi Marshall Orson, wote wawili watatoa hotuba wakiwa na wanachama wa ziada wa bodi na familia ya Watson-Harris. Kutokana na ugonjwa wa COVID-19 unaoendelea, watu watakaohudhuria hafla hiyo watakuwa wachache, na wale watakaohudhuria watazingatia maagizo ya sasa ya kujitenga na watu. Utiririshaji wa moja kwa moja wa hafla hiyo unaweza kutazamwa kuanzia saa 9:30 asubuhi kwenye [tovuti ya DCSD](#). Picha na video zitapatikana baada ya hafla hiyo kukamilika.

Halmashauri ilipiga kura 6 -1 mwezi wa Juni 18 ya kumteua Watson-Harris, mshindani wa pekee wa Wilaya, kama msimamizi anayefuata na atekeleze mkataba wa ajira wa miaka tatu. Katika siku zijazo atakuwa akikutana na viongozi wa wilaya, wafanyakazi na wanajamii.

Watson-Harris atachukua nafasi ya Ramona Tyson, ambaye amehudumu kama msimamizi wa muda na msimamizi tangu Novemba 2019. Baada ya miongo mitatu ya huduma ya kipekee ya DCSD, atastaafu mnamo Juni 30.

KUTUHUSU: Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb hutumia Mafunzo na Elimu ya Kina (Deep Teaching and Learning) kuwanda zaidi ya wanafunzi wake 102,000 kwa chuo cha elimu na kazi. Mafunzo na Elimu ya kina huwafunza wanafunzi kufikiria kwa umakinifu, kutatua matatizo, kuwasiliana, na kushirikiana vizuri ili kufanikiwa katika chuo cha elimu, kazi, na maisha. Kujifunza zaidi, tembelea www.dekalbschoolsga.org. Wasilisha maswali au maoni kwa Communications@dekalbschoolsga.org.